**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU L. NCHEMBA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUAHIRISHA MKUTANO WA 2 WA BUNGE LA 13 LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 06 FEBRUARI 2026 JIJINI DODOMA**

## UTANGULIZI

### Shukrani na Pongezi

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema hadi leo hii tunapohitimisha shughuli zote zilizopangwa katika mkutano huu wa pili wa Bunge la 13**.**

### Pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kupitia Bunge lako tukufu nimshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na juhudi zake za kuwatumikia wananchi kwa mapenzi ya dhati**.** Sote ni mashahidi na tunatambua kazi kubwa anayoifanya katika maendeleo ya Taifa letu. Uongozi wake unaendelea kuwa chachu ya matumaini na dira ya mwelekeo wa Taifa.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumtakia Mheshimiwa Rais afya njema, hekima na nguvu zaidi katika kutekeleza majukumu yake makubwa ya kuliongoza Taifa letu.

### Pongezi kwa Mheshimiwa Spika

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii kukupongeza sana wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kazi kubwa na nzuri ya kuliongoza Bunge. Wakati wa kipindi chote cha mkutano huu wa pili, tumeshuhudia mkiongoza mijadala yote kwa umahiri wa hali ya juu. Sina shaka, Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana nami kuwa mafanikio ya mkutano huu yametokana na weledi mkubwa wa Mheshimiwa Spika na wasaidizi wake katika kusimamia shughuli za Bunge. **Ninakupongeza sana Mheshimiwa Spika!**

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge kwa pongezi zenu kwa Serikali na kwa michango yenye dhamira ya dhati ya kuboresha mipango na kazi zinazokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika kipindi hiki cha miaka mitano. Mjadala huu umeendelea kuthibitisha uimara wa Bunge katika kutekeleza wajibu wake wa Kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali kikamilifu. Michango na maoni yenu katika mkutano huu imepokelewa na itafanyiwa kazi na Serikali.

### Pongezi kwa Teuzi Mbalimbali

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** tangu alipoapishwa na kuingia madarakani, Mheshimiwa Rais amefanya teuzi ambazo zimelenga kuimarisha utendaji na utoaji huduma kwa wananchi. Nitumie nafasi hii kuwapongeza Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wengine walioteuliwa kwenye nyadhifa mbalimbali.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb), Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.) na Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Vilevile, ninawapongeza kwa kazi kubwa ya kukusaidia katika kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge hili.

Ninapenda pia kutumia fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuwa Wenyeviti na Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge.

**Salamu za Pole Kufuatia Matukio Mbalimbali**

**8.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa masikitiko makubwa, ninaungana tena na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwa Bunge lako tukufu kutokana na vifo vya wabunge wenzetu wawili. Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye alikuwa Mbunge wa Peramiho, aliyeaga dunia tarehe 11 Desemba, 2025 jijini Dodoma. Pia, Mheshimiwa Halima Idd Nassor Mbunge wa Viti Maalum, aliyeaga dunia tarehe 18 Januari, 2026 Jijini Dar es Salaam. Wakati wote tutaendelea kukumbuka mchango wao katika maendeleo ya Taifa letu. Mwenyezi Mungu awape pumziko la amani. **Amina!**

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wenzetu waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki na wengine waliopata madhara mbalimbali kutokana na ajali za barabarani na matukio mengine. Ninamuomba Mwenyezi Mungu awape subira waliopoteza ndugu, majeruhi wapone kwa haraka na marehemu wote wapumzike kwa amani. **Amina!**

**SHUGHULI ZA BUNGE**

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** mkutano huu kimsingi ni wa kwanza kujadili taarifa mbalimbali za Serikali katika Bunge la 13. Nimefurahishwa na namna Waheshimiwa Wabunge wenzangu mlivyotoa michango na ushauri wenu kwenye shughuli za Kibunge. ***Hongereni sana Wabunge wenzangu!!***

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na shughuli nyingine za bunge, mkutano wa pili wa Bunge la 13, ulipokea na kujadili taarifa zifuatazo: -

i. Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa ufunguzi wa Bunge la 13;

ii. Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027 – 2050/2051;

iii. Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031;

iv. Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa fedha 2026/2027; na

v. Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika muda wa kati ya 2026/2027 – 2028/2029.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge waliuliza maswali **.......** ya msingi na mengine **......** ya nyongeza ambayo yalijibiwa na Serikali. Halikadhalika, maswali **saba** ya papo kwa papo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Waziri Mkuu.

**MICHANGO YA WABUNGE**

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imefuatilia kwa makini mijadala ya Waheshimiwa Wabunge, ambapo hoja zilizotolewa zimeonesha wazi kuunga mkono juhudi kubwa za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu**

**Hassan** katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Wakati huohuo, Waheshimiwa Wabunge wameeleza matarajio yao ya kuona miradi hiyo, hususan ya maji, nishati, barabara na miundombinu mingine, inakamilika kwa haraka ili wananchi waanze kunufaika kikamilifu.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** tayari nimewaelekeza Mawaziri wa Fedha, Ujenzi, Maji, Nishati pamoja na TAMISEMI kuandaa mchanganuo wa kina wa miradi yote iliyoidhinishwa na inayoendelea kutekelezwa kwa kusuasua au kusimama. Mchanganuo huo pia uhusishe miradi iliyosainiwa na haijaanza kutekelezwa, na ile ambayo hati zake zimewasilishwa na malipo hayajafanyika ili kuweka mkakati madhubuti wa kukamilisha malipo na hatimaye kuharakisha utekelezaji wake kwa wakati.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa maelekezo mahsusi kwa Waheshimiwa Mawaziri husika kuhakikisha zoezi hili linakamilika kabla ya kuanza kwa Vikao vya Bunge la Bajeti, ili hoja za Waheshimiwa Wabunge zichukuliwe hatua kwa vitendo na miradi ikamilike kwa viwango vinavyotarajiwa.

**MPANGO NA BAJETI**

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** utakumbuka kuwa, tarehe 02 Februari, 2026 Waziri wa Mipango na Uwekezaji na Waziri wa Fedha waliwasilisha Bungeni Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/2027 – 2050/2051; Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031; Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika muda wa Kati wa 2026/2027 – 2028/2029; na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/2027.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (2026/2027–2050/2051), umeainisha malengo mahsusi na afua kwa kuzingatia shabaha na vipaumbele vilivyoainishwa katika Dira 2050. Kwa kuzingatia ongezeko la watu nchini na athari zake katika upatikanaji wa ardhi, huduma za jamii na miundombinu, umuhimu wa kuharakisha mageuzi ya kiuchumi na kukuza uwekezaji nchini, Mpango Elekezi umeweka mkazo maalum katika mambo sita yafuatayo:

**Moja:** Upangaji miji endelevu na unaozingatia utunzaji wa mazingira;

**Mbili:** Ushirikishwaji mpana katika kupanga mipango ya maendeleo;

**Tatu:** Kuongeza wigo na ubora wa huduma za jamii;

**Nne:** Kuongeza tija katika kilimo, uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma kwa kuongeza kasi ya matumizi ya teknolojia (ikiwemo matumizi ya dijitali), ubunifu na uongezaji thamani mazao mbalimbali;

**Tano:** Kuweka mazingira rafiki na yanayotabirika ya uwekezaji na kufanya biashara ili kuvutia mitaji kutoka sekta binafsi ya ndani na nje ya nchi; na

**Sita:** Kufanya mageuzi katika mfumo wa utawala na mabadiliko ya utamaduni na mitazamo.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/2027 – 2030/2031, una dhima ya Mageuzi kwa Ajili ya Ukuaji wa Uchumi Jumuishi

na Uzalishaji wa Ajira. Hatua hii, itaweka msukumo wa kipekee katika kutekeleza mageuzi makubwa yatakayobadilisha mifumo, mitazamo na mwenendo katika utendaji ili kuchochea tija katika uzalishaji, kuongeza uwezo wa nchi katika kushindana kikanda na kimataifa, na kuchochea muunganiko wa sekta mbalimbali. Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafiri na usafirishaji wa bidhaa, viwanda na biashara katika ukanda wa Afrika.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027, ni ya kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maeneo ya kimkakati yanayopendekezwa kupewa kipaumbele katika Mpango huo ni yafuatayo:

**Moja:** Kujenga uchumi imara, jumuishi na shindani kwa kufanya mageuzi ya mifumo ya utendaji wa taasisi na kuimarisha utawala bora;

**Mbili:** Kuimarisha uwezo wa watu na maendeleo ya kijamii ili kuwa na watu wenye ujuzi, afya na wanaoweza kuhimili mabadiliko;

**Tatu:** Kuimarisha miundombinu ya kidijitali, nishati, na usafirishaji fungamanishi;

**Nne:** Kuimarisha sekta zinazochochea uzalishaji, uongezaji thamani na ukuaji jumuishi; na

**Tano:** Kuimarisha uhifadhi wa mazingira na uwezo wa nchi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika muda wa Kati ya 2026/2027 – 2028/2029, Serikali itatekeleza vipaumbele katika miradi inayoendelea, iliyosainiwa pamoja na vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Maeneo mahsusi ya kipaumbele katika matumizi ni kugharimia miradi ya kielelezo na kimkakati inayoendelea, deni la taifa, mishahara ya watumishi wa umma na huduma za jamii. Katika maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2026/2027, maelekezo ya kimkakati kwa Maafisa Masuuli ambayo yanapaswa kuwa na msukumo ni pamoja na:-

**Moja:** Kwakuwa serikali imepanga kuongeza asilimia tano kwenye Mikopo ya Wanawake, Vijana na Wenye ulemavu inayotokana na mapato ya ndani ya halmashauri, ninaelekeza Ofisi za Wakuu wa Mikoa kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutumia kwa pamoja asilimia tano kati ya asilimia 15 ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya kuboresha mazingira ya biashara na ujasiriamali ili kuvutia na kuongeza fursa za ajira kwa makundi haya;

**Mbili:** Maafisa Masuuli kuzingatia mkakati wa kulinda wawekezaji wa ndani kwa kutoa kipaumbele cha kwanza katika zabuni, masharti ya mikataba na malipo ya hati za madai;

**Tatu:** Maafisa Masuuli kuandaa mikakati ya kuzalisha, kulea na kukuza wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa kupitia dhana ya ushirikishaji wa wananchi katika utekelezaji, uwezeshaji na upatikanaji wa mikopo ya gharama nafuu ili kuwezesha uibuaji wa fursa za ajira hususan kwa vijana; na

**Nne:** Taasisi na mashirika ya umma hususan yanayojiendesha kibiashara yaweke mikakati ya kuondokana na utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu ifikapo Juni 2029 ili kutoa fursa ya serikali kuendelea .....;

**Tano:** Mamlaka za Serikali za Mitaa kuongeza uwazi katika utekelezaji wa miradi katika halmashauri zetu. Mapato yote yajulikane kwa waheshimiwa wabunge na madiwani. Kila wakati, Katibu Tawala Mkoa anapotuma fedha kwenye halmashauri atoe nakala kwa ofisi ya mkuu wa wilaya, ofisi ya mbunge, ofisi ya meya, wenyeviti wa halmashauri na madiwani na aainishe aina ya miradi inayoenda kutekelezwa.

Ratiba ya vikao vya baraza la madiwani izingatie ratiba ya vikao vya bunge ili kutoa fursa kwa wabunge kushiriki kwa vile vikao vya Bunge si vya dharura na ratiba yake inajulikana mapema. Miradi yote ambayo ipo kwenye hatua za utekelezaji gharama zake zisiwe siri, taarifa zake zijulikane kwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Wabunge, Meya, Wenyeviti wa Halmashauri na Madiwani. Lengo la kuweka uwazi ni kuwarahisishia Waheshimiwa Wabunge kufuatilia miradi inayotekelezwa kwenye maeneo yao.

Ili kufanikisha utekelezaji wa maelekezo hayo Ninawaomba waheshimiwa wabunge mnaporejea majimboni fuatilieni kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, wekeni mawe ya msingi na zindueni miradi hiyo. Vilevile hakikisheni mnapata taarifa za utekelezaji wa kila mradi na maeneo ambayo mnaushauri tumieni fursa zote zikiwemo vikao vya halmashauri, vikao vya baraza la ushauri la wilaya (DCC), vikao vya Baraza la Ushauri la Mkoa (RCC), wizara za kisekta au hata Ofisi ya Waziri Mkuu; na

**Sita:** Kwa kuwa mchango wa Sekta Binafsi katika utekelezaji Dira ya Taifa ni mkubwa, nitoe rai kwa viongozi na watendaji wote wa serikali kuhakikisha mnaithamini na kuishirikisha sekta binafsi katika hatua mbalimbali za kupanga na kutekeleza miradi yote ya maendeleo. Sekta binafsi ipewe heshima ili kuhakikisha mchango wao unaonekana.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako limepata muda wa kuchangia na kuishauri Serikali juu ya Mpango na Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti kama ilivyowasilishwa hapa Bungeni. Aidha, tunaliahidi Bunge lako kuwa tutafanyia kazi maoni na ushauri wote uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

**MAFANIKIO YA MHESHIMIWA RAIS**

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** sote tunakumbuka kuwa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania alitoa ahadi mbalimbali kwa wananchi. Ahadi hizo ni pamoja na zile zitakazotekelezwa ndani ya siku 100 baada ya Serikali kuingia madarakani.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** ahadi za Mheshimiwa Rais zinaendelea kutekelezwa kikamilifu na Waheshimiwa Mawaziri wa Kisekta wamekuwa wakitoa taarifa za utekelezaji na mafanikio yaliyopatikana. Nami nitumie fursa hii kueleza kwa muhtasari mafanikio hayo kama ifuatavyo:

**Afya**

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika sekta ya afya, serikali imepata mafanikio makubwa ikiwemo kuongeza wigo wa upatikanaji na ufanisi wa utoaji wa huduma za afya nchini. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya ni pamoja na yafuatayo:-

i. Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Wote kwa awamu ya majaribio ambao unahusisha makundi maalum ya watoto, wajawazito na wenye ulemavu;

ii. Kugharimia kwa asilimia 100 matibabu ya vipimo vya kibingwa kwa magonjwa sugu yasiyoambukiza yakiwemo saratani, figo, moyo, sukari, mifupa na mishipa ya fahamu;

iii. Kuondoa zuio la kuchukua miili ya marehemu katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kwa kigezo cha madeni ya matibabu na kufanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya afya;

iv. Kuajiri watumishi wa afya 5,000 na kuwapangia vituo vya kazi kote nchini;

v. Kutoa zaidi ya shilingi bilioni 39 ili kuboresha huduma za uzazi na watoto wachanga katika vituo 89 vya kutolea huduma za afya;

vi. Kuongeza vituo vya upasuaji wa dharura kutoka vituo 523 Oktoba, 2025 hadi vituo 578 Januari, 2026; na

vii. Kuongeza uwezo wa Taifa kukabiliana na athari za VVU na UKIMWI kwa kuhakikisha utoshelevu wa dawa za kufubaza makali ya UKIMWI kwa kufufua Kiwanda cha *Tanzania Pharmaceutical Industries (TPI)* kilichopo mkoani Arusha na kuongeza fedha za ndani kupitia Mfuko wa Udhamini wa Afua za UKIMWI.

**Elimu**

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora katika ngazi mbalimbali. Lengo ni kuwezesha wanafunzi wa Kitanzania kupata ujuzi utakaomudu ushindani Kitaifa na Kimataifa. Hivyo, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na yafuatayo:

i. Kuzindua Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) unaolenga kuhakikisha mtoto wa darasa la tatu anasoma, anaandika na anahesabu bila shida;

ii. Kuajiri na kuwapangia vituo vya kazi jumla ya **walimu 7,000** wa masomo ya Sayansi na Hisabati;

iii. Kukamilisha mpango wa pamoja kati ya Waajiri, Vyuo vya Ufundi Stadi na Vyuo Vikuu kwa lengo la kulinganisha mafunzo na mahitaji ya sekta za kipaumbele;

iv. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA shuleni kwa kusambaza vifaa katika shule za msingi na sekondari;

v. Kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu kwa kuendelea kutoa mikopo ya elimu ya juu kupitia mikopo ya wanafunzi pamoja na ufadhili na kutekeleza mpango wa elimu bila ya ada kwa shule za msingi na sekondari; na

vi. Kuendeleza tafiti na bunifu kupitia mfuko maalum wa ***Samia Commercialization Fund*** ili kubidhaisha bunifu na teknolojia.

**Maji**

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha upatikanaji wa maji ya uhakika kwa matumizi ya nyumbani, kilimo, mifugo na shughuli nyingine za kiuchumi, serikali imetekeleza yafuatayo:-

i. Ujenzi wa Gridi ya Taifa ya Maji kwa kukamilisha usanifu na upembuzi yakinifu wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo ule wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi Dodoma kupitia Singida, pamoja na miradi ya kupeleka maji ya mto Rufiji katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Lindi na mto Ruvuma katika Halmashauri ya Mtwara Mikindani;

ii. Kuendeleza maandalizi ya miradi ya kupeleka maji kutoka Ziwa Tanganyika kwenda mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa;

iii. Kufanikisha kukamilika kwa **miradi 16** ya maji na kuendelea na ujenzi wa **miradi 71** mingine ya maji itakayonufaisha zaidi ya wananchi **milioni tatu** nchini; na

iv. Kulipa fidia kwa wananchi na kusaini mikataba ya kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Geita, Singida, Mwanza na Morogoro.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua dhamira na msisitizo wa Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa Watanzania, tarehe 02 Januari, 2026 nilifanya ziara ya kutembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa Bwawa la Kidunda, ambapo nilijionea binafsi hatua iliyofikiwa ya utekelezaji ambayo ni asilimia 40.13. Hakika, mradi huu ukikamilika utaenda kutatua changamoto ya maji kwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro (Ngerengere na Gwata) pamoja na maeneo ya Mkoa wa Tanga (Kwasunga kule Handeni).

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua kazi kubwa ya Mheshimiwa Rais kuhusu mradi huo nilielekeza Wizara ya Fedha na Wizara ya Maji kuharakisha malipo ya hati zilizokuwa zimewasilishwa ya kiasi cha shilingi **bilioni 24.83**. Nimepata taarifa kwamba kiasi hiki tayari kimeshwalipwa tarehe 31 Januari, 2026. Nielekeze wizara ya maji kuendelea kusimamia kwa ukaribu utekelezaji wa mradi huo ili ukamilike kwa wakati kama yalivyo maelekezo ya Mheshimiwa Rais.

**Nishati**

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika sekta ya nishati, serikali imeendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia na kupata mafanikio makubwa. Mafanikio haya yanaimarisha upatikanaji wa nishati ya uhakika kwa matumizi ya kijamii na kiuchumi na kuharakisha maendeleo ya Taifa. Sambamba na hilo, serikali imefanikisha masuala yafuatayo:-

i. Kuwezesha upatikanaji wa majiko banifu na mitungi ya gesi ya LPG kwa ruzuku;

ii. Kuendelea kuhamasisha taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku kuhamia katika matumizi ya nishati safi;

iii. Ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia na kuanza kuunganisha katika nyumba kwenye mikoa ya Lindi na Pwani;

iv. Kuandaa mazingira ya uzalishaji wa nishati mbadala kupitia mitambo ya mkaa mbadala katika mikoa ya Tabora na Dodoma;

v. Kutekeleza miradi ya kuunganisha umeme kwa wateja wapya;

vi. Kukamilisha awamu ya kwanza ya mradi wa kuzalisha umeme wa jua wa megawati 50 wilayani Kishapu mkoani Shinyanga utakaounganishwa katika Gridi ya Taifa; na

vii. Kuendelea kutekeleza miradi ya kupeleka umeme katika vitongoji 9,009 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.2 kama tulivyoshuhudia utiaji saini wake ukifanyika.

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**30.** ***Mheshimiwa Spika*, **Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuwawezesha wananchi kiuchumi. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na zifuatazo: -

i. Kuongeza upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya biashara ndogo za kati na kampuni changa. Tarehe 05 Februari, 2026 nilishiriki kwenye tukio muhimu la uzinduzi wa utoaji mitaji yenye thamani ya **shilingi bilioni 200** ili kuwawezesha wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara, maafisa usafirishaji, wasanii na kampuni changa za vijana kuongeza mitaji, kukuza biashara na kuchangia ajira na ukuaji wa uchumi;

ii. Kutoa mikopo mingine yenye masharti nafuu kupitia mifuko mbalimbali na kunufaisha wafanyabiashara wadogo, wajasiriamali na kampuni changa; na

iii. Kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo zaidi ya milioni moja na kuwapatia mikopo yenye thamani ya shilingi **bilioni 707.4** kutoka taasisi za fedha za NMB, DCB na TCB.

**Mafanikio Mengine.**

**Fedha**

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Sekta ya Fedha, Serikali imeendelea kuboresha usimamizi wa mapato na uthabiti wa uchumi. Maboresho hayo yamewezesha kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya ndani na kuvuka malengo yaliyowekwa. Hatua hiyo imewezesha Serikali kutekeleza ahadi mbalimbali zilizotolewa na Mheshimiwa Rais ikiwemo kugharimia huduma za jamii, miradi ya maendeleo na kuwanufaisha wananchi.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** mathalan, katika kipindi cha Novemba hadi Desemba, 2025 Mamlaka ya Mapato Tanzania, imekusanya shilingi trilioni 6.99 sawa na asilimia 101.89 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 6.86.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** nazielekeza Wizara za Kisekta ambazo hazijakamilisha utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha Mpango wa utekelezaji wake unakamilika kwa wakati. Kukamilika kwa utekelezaji wa ahadi hizo iwe ni kigezo cha utendaji ndani ya Serikali. Pia, ziendelee kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa kujenga miundombinu na kutatua kero za wananchi.

**KILIMO**

**Hali ya Mwenendo Mvua na Mazao**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini ilitoa utabiri wa mwelekeo wa msimu wa mvua za vuli kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Desemba, 2025 na mwelekeo wa mvua za msimu zinazoanza Novemba, 2025 hadi Aprili, 2026. Kama ilivyotabiriwa, mvua za vuli zilikuwa chini ya wastani katika baadhi ya maeneo na hivyo kuathiri ukuaji wa mazao na mavuno. Hata hivyo, kipindi cha nusu ya

pili ya msimu wa mvua mwezi Februari, 2026 hadi Aprili, 2026 kinatarajiwa kuwa na ongezeko la mvua ikilinganishwa na nusu ya kwanza.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla hali ya mazao shambani inaendelea vizuri na mazao mengi yapo katika hatua za ukuaji. Katika maeneo yanayopata mvua za vuli baadhi ya mazao yameanza kuvunwa hususan mahindi na maharage. Kadhalika, mazao mengine yapo katika hatua mbalimbali za ukuaji na yanaendelea vizuri.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwaelekeza maafisa ugani kuendelea kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakulima kwa wakati. Aidha, niwakumbushe wakulima kuhakikisha wanazalisha mazao yanayokomaa kwa muda mfupi kulingana na kanda za uzalishaji ili kuwa na uhakika wa utoshelevu wa chakula.

**Hali ya Upatikanaji wa Chakula**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya upatikanaji wa chakula nchini ni ya kuridhisha. Hii imetokana na uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo 2024/2025 kuwa mzuri ambapo uzalishaji ulifikia tani milioni 23.8 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 18.3. Uzalishaji huo umeihakikishia nchi utoshelevu wa chakula kwa asilimia 130. Pamoja na hatua hiyo nzuri ya upatikanaji wa chakula nchini, bado kuna maeneo ambayo uzalishaji wake haukuwa wa kuridhisha. Hivyo, Serikali inaendelea na tathmini ya kina kubaini hali ya chakula katika maeneo hayo na kuchukua hatua stahiki.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** akiba ya chakula ya Taifa imeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia mwezi Desemba 2025, akiba ya chakula kilichohifadhiwa na Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula kimefikia tani 578,072. Kuimarika kwa usalama wa chakula nchini kumetokana na uzalishaji mzuri wa mazao ya chakula uliochangiwa na jitihada mbalimbali za Serikali ikiwemo utoaji wa ruzuku za pembejeo za kilimo, kuimarishwa kwa miundombinu ya umwagiliaji, huduma za ugani, zana bora za kilimo na upatikanaji wa mbegu bora.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** jitihada hizo zinatokana na maono na dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuendeleza kilimo na kuwasaidia wakulima nchini. Pamoja na jitihada hizo, hivi karibuni ameridhia utekelezaji wa mkakati wa Taifa wa Zana za Kilimo unaolenga kuimarisha matumizi, uzalishaji, usimamizi na uratibu wa teknolojia za kilimo katika mnyororo mzima wa thamani.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia mkakati huo serikali imepanga kununua matrekta 10,000 na kuanzisha vituo jumuishi 1,000 vya huduma za zana za kilimo katika ngazi ya kata. Hivyo, utekelezaji wa mkakati huo utaleta mageuzi makubwa katika sekta ya kilimo na kuwanufaisha wakulima. ***Hakika Mheshimiwa Rais anastahili pongezi!!***

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie Bunge lako tukufu, kuielekeza Wizara ya Kilimo kuendelea kusimamia kikamilifu sekta ya kilimo ikiwemo miradi ya umwagiliaji, kuongeza thamani ya mazao na uhifadhi wa mazao. Aidha, niwakumbushe Maafisa Ugani na Maafisa Kilimo kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kanuni bora za kilimo na matumizi ya teknolojia za uhifadhi wa mazao. Kwa upande mwingine, nitoe wito kwa wakulima kutumia vizuri mavuno wanayopata sambamba na kuzingatia maelekezo ya wataalam.

**Usimamizi wa Elimumsingi**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na uandikishaji wanafunzi wa darasa la awali, darasa la kwanza na wanafunzi wanaosoma kupitia Mpango wa Elimu Msingi Kwa Waliokosa (MEMKWA). Hadi tarehe 23 Januari 2026, idadi ya wanafunzi wa darasa la awali walioandikishwa ni 1,049,015 (wavulana 522,267 na wasichana 526,748) wakiwemo wenye mahitaji maalum 1,316 (wavulana 716 na wasichana 600).

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hao, idadi ya wanafunzi wa darasa la kwanza walioandikishwa ni 1,341,112 (wavulana 665,936 na wasichana 675,176) wakiwemo wenye mahitaji maalum 2,080 (wavulana 1,137 na wasichana 943).

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa elimu ya sekondari, idadi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza walioripoti hadi kufikia tarehe 23 Januari, 2026 ni 510,474 (Wavulana 234,389 na Wasichana 276,085) wakiwemo wenye mahitaji maalum 1,116 (Wavulana 571 na Wasichana 532). Aidha, wanafunzi walioripoti ni sawa na asilimia 54.45 ya wanafunzi 937,581 waliochaguliwa.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya wanafunzi walioripoti kidato cha kwanza hadi sasa bado hairidhishi, nitoe maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuhakikisha watoto wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaripoti shuleni. Vilevile, nitoe wito kwa wazazi na walezi wenye watoto walio na sifa ya kuandikishwa darasa la awali au la kwanza wahakikishe wanawapeleka watoto shuleni kuandikishwa kwa mujibu wa sheria ili kutekeleza kwa vitendo azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa hakuna mtoto wa kitanzania anayekosa elimu.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufaulu wa wanafunzi wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne umekuwa ukiongezeka ambapo kwa mwaka 2025 jumla ya watahiniwa wa shule 526,620 kati ya 555,606 sawa na asilimia 94.98 walifaulu Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne ikilinganishwa na mwaka 2024 ambapo watahiniwa 440,847 kati ya 477,262 walifaulu sawa na asilimia 92.37.

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo haya yametokana na Serikali kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule zetu ikiwemo kununua na kusambaza vitabu milioni 18 vya ziada. Vilevile, Serikali imenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia vyenye thamani ya shilingi bilioni 5.4 pamoja na vifaa vya TEHAMA. Sambamba na hilo Serikali imewezesha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ikiwemo mabweni, madarasa, mabwalo ya chakula, nyumba za walimu kwa shule za msingi na sekondari.

**Masuala ya Msisitizo**

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii mbele ya Bunge lako tukufu kuweka msisitizo kuhusu maeneo muhimu ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu kama ifuatavyo:

**Kuimarisha Utekelezaji wa Miradi kwa Ubia**

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali haiwezi kutekeleza miradi yote ya maendeleo kwa wakati kwa kutegemea rasilimali za serikali peke yake. Sekta binafsi ni mdau mkubwa katika maendeleo na injini ya kuchachusha utekelezaji wa miradi mbalimbali. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa ubia. Kwa msingi huo ninaelekeza yafuatayo:

**Mosi:** Wizara ya Fedha kupitia Kituo cha Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Ubia uhakikisha kinaratibu Sekta zote na kutoa ridhaa kwa miradi yote inayokidhi vigezo ya kuendeshwa kwa ubia; na

**Pili:** Maafisa Masuuli wote wahakikishe wanatoa kipaumbele na ushirikiano kwa Sekta Binafsi zenye uwezo na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa ubia.

**Kuimarisha amani, usalama na utulivu**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** amani, usalama na utulivu ni jukumu la kila mtanzania na linahitaji juhudi za pamoja katika nyanja mbalimbali. Hivyo tunawajibika kuepuka masuala yote yanayochochea uvunjifu wa amani yetu ikiwemo matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii. Pamoja na jukumu hili, ninapenda kukumbusha masuala muhimu yafuatayo: -

**Mosi:** Wizara yenye dhamana na Ustawi wa Jamii iweke kipaumbele kwa kushirikiana wadau mbalimbali wakiwemo Viongozi wa Asasi za Kiraia na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kutoa elimu ya malezi bora katika jamii;

**Pili:** Ninawaasa Watanzania wenzangu kuwa na matumizi chanya ya mitandao ya kijamii na kuifanya kuwa nyenzo muhimu ya kujielimisha, kuendeleza biashara na kukuza uchumi; na

**Tatu:** Nitoe rai kwa Watanzania wote kulinda Tunu za Taifa kwa kuwa ni wajibu wa kila raia, kuziheshimu na kuziendeleza ili kuleta mshikamano na kuimarisha heshima ya taifa letu.

**Maridhiano**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** sote tunatambua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa mstari wa mbele katika kuleta mshikamano na maridhiano. Hii inajidhihirisha kupitia maamuzi yake ya kuunda Tume Huru ya Uchunguzi wa Matukio ya Uvunjifu wa Amani yaliyotokea wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu. Mapendekezo ya Tume hiyo yataweka msingi kuelekea uundwaji wa Tume ya Mazungumzo na Maridhiano kama alivyoahidi kuiunda.

**Kukamilisha utekelezaji wa miradi ya Serikali**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali sikivu ya Awamu ya Sita itaendelea kukamilisha miradi yote iliyoanza kutekelezwa ili ilete tija kwa wananchi. Hivyo, nawaelekeza Maafisa Masuuli kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango kukamilisha Miradi iliyopo kwenye Mafungu yao. Aidha, sekta binafsi ishirikishwe kikamilifu kwa miradi ya kielelezo yenye manufaa na matokeo makubwa inayohitaji teknolojia na utaalam wa sekta binafsi.

**Kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi 2025**

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa siku ya Jumatatu, tarehe 03 Novemba 2025, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliapishwa rasmi kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uapisho wa Mheshimiwa Rais, ni ishara ya kuanza utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba Serikali itatekeleza

kikamilifu ilani kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwenye kila Ibara kwa lengo la kukamilisha Kauli Mbiu ya "***Kazi na Utu, Tunasonga Mbele***".

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** niendelee kuwasisitiza Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watumishi wa umma watenge muda wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi katika maeneo yao hususan kwenye migogoro ya ardhi. Wafuateni, wasikilizeni na tatueni kero zao ili wasilazimike kwenda ngazi za juu au kusubiri ziara za viongozi wa kitaifa kwa masuala ambayo mngeweza kuyafanyia kazi.

**Michezo**

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imeendelea kufanya vizuri katika michezo mbalimbali. Mafanikio hayo yanatokana na maono na uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo katika uongozi wake, tumeshuhudia mageuzi makubwa katika sekta ya michezo nchini. Kutokana na hatua hizo, timu zetu za ngazi mbalimbali zimeendelea kufanya vizuri na kulitangaza Taifa letu kitaifa, kikanda na kimataifa.

**56.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii adhimu kuipongeza Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu – Taifa Stars kwa kufanikiwa kuandika historia kwa kufuzu hatua ya 16 Bora ya Michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025. Tangu kuanzishwa mashindano haya, Tanzania imefanikiwa kushiriki mara nne (4): mwaka 1980 nchini Nigeria; mwaka 2019 nchini Misri; mwaka 2023 nchini Ivory Coast; na mwaka 2025 nchini Morocco ambapo tumeweka rekodi ya kuingia 16 bora. Mashindano ya AFCON hutazamwa na watu wengi duniani, hivyo, mafanikio haya yameiwezesha Tanzania kutambulika zaidi katika ramani ya soka barani Afrika na duniani kote.

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, Baraza la Michezo la Taifa, benchi la ufundi, wachezaji pamoja na wadau wa michezo imeelekeza nguvu katika maandalizi ya Taifa Stars ili kuhakikisha inafanya vizuri zaidi katika mashindano yajayo ya AFCON 2027 yatakayofanyika kwa umoja nchini Tanzania, Kenya na Uganda. Aidha, Maandalizi ya miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi na ukarabati wa viwanja yanaendelea vizuri. Matarajio yetu ni kuhakikisha maandalizi yanafanyika kwa ufanisi na kombe hilo linabaki nchini. Nitoe wito kwa Watanzania wote kuendelea kuiunga mkono timu yetu ya Taifa wakati wote na kuchangamkia fursa mbalimbali zitakatojitokeza wakati wa maandalizi na kipindi cha mashindano.

**58.** ***Mheshimiwa Spika***, Pia, timu zetu za taifa za michezo mingine zimeendelea kufanya vizuri katika maeneo mbalimbali mathalan, katika mchezo wa kriketi, Timu ya Taifa ya Vijana chini ya umri wa miaka 19 ilifanikiwa kufuzu mashindano ya Kombe la Dunia la Kriketi chini ya umri wa miaka 19 yaliyofanyika mwezi Januari 2026 nchini Namibia, hatua muhimu katika maendeleo ya mchezo huo nchini. Aidha, Timu nyingine za Taifa zilizofuzu katika hatua mbalimbali za mashindano ya Kimataifa ni pamoja na: Timu ya Taifa ya wanawake ya *Futsal*; Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu wanawake "Twiga Stars"; Klabu ya JKT Queens; Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu chini ya umri wa miaka 20 (*Ngorongoro Heroes*); Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu (*Tembo Warriors*); Timu ya taifa ya ngumi; Timu ya taifa ya kuogelea; na Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu chini ya umri wa miaka 17 (*Serengeti Boys*).

**59.** ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda pia kuzipongeza klabu zetu za soka nchini kwa mafanikio makubwa wanayoendelea kuyapata katika mashindano ya kimataifa. Klabu za michezo za Simba na Yanga zimeonesha ushindani wa hali ya juu kwa kufanikiwa

kufuzu na kushiriki katika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Barani Afrika, hali inayodhihirisha uimara, ubora na ukuaji wa soka la Tanzania katika ngazi ya Afrika. Aidha, klabu za Azam na Singida Big Stars nazo zimefanikiwa kufuzu na kushiriki hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Barani Afrika. Mafanikio haya yameendelea kuitangaza vyema nchi yetu, kuipa heshima kubwa kimataifa, pamoja na kuongeza alama na nafasi ya Tanzania katika viwango vya soka la Afrika.

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, katika hatua ya kuendeleza na kukuza vipaji vya michezo, hususan miongoni mwa vijana wetu, Serikali inaendelea kutekeleza kwa kasi ujenzi wa Akademia ya Michezo ya Malya. Mradi huu ni moja ya uwekezaji mkubwa wa kimkakati unaolenga kuandaa kizazi kipya cha wanamichezo mahiri watakaoweza kushindana katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa. Akademia hii itatumika kwa ajili ya kambi ya timu ya taifa wakati wa maandalizi ya AFCON, 2027.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuipongeza klabu ya Yanga kwa kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Kombe la Mapinduzi, katika fainali iliyochezwa katika Uwanja wa Gombani, Pemba, dhidi ya klabu ya Azam. Mashindano ya Kombe la Mapinduzi si tu burudani, bali yamekuwa chachu ya mshikamano wa kitaifa, umoja, na kukuza vipaji vya michezo nchini.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inatambua na kuthamini mchango wa wanamichezo wetu binafsi katika kulitangaza Taifa. Ninapenda kumpongeza mwanariadha wetu mashuhuri Alphonce Simbu, kwa kuwa bingwa wa Dunia wa marathon katika mashindano ya riadha yaliyofanyika jijini Tokyo nchini Japan ambapo alinyakua medali ya dhahabu. Mafanikio hayo yameitangaza Tanzania kimataifa na kuipa heshima taifa letu.

**Shukrani na Kutoa Hoja**

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** nihitimishe hotuba yangu kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu muhimu mliyoitoa kwa lengo la kuboresha maisha ya wananchi wetu. Kama nilivyotangulia kusema, michango yenu ni muhimu sana katika kuimarisha utendaji wa Serikali.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Katibu wa Bunge, wasaidizi wake na watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri na msaada mkubwa ambao wamekuwa wakitupatia kwa kipindi chote tulichokuwa tukitekeleza majukumu yetu ya Mkutano wa Pili wa Bunge la 13. Kadhalika ninavishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri ya kuhakikisha usalama wa waheshimiwa wabunge na wageni wetu na hatimaye leo tunahitimisha mkutano huu kwa amani.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na watumishi wote wa Serikali. Mmefanya kazi kubwa na nzuri na mmekuwa mkitoa ufafanuzi unaohusu sekta zenu kwa wakati na kwa weledi. Utendaji wenu umekuwa chachu ya mafanikio ya mijadala ya Waheshimiwa Wabunge.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru pia viongozi na watendaji wa Serikali na taasisi zake ambao wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa weledi, umahiri na ufanisi mkubwa. Hongereni sana kwani juhudi zenu zimekuwa chachu ya kufanikisha shughuli zilizopangwa kwenye mkutano huu. Vilevile, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitowashukuru wanahabari kwa uchambuzi mzuri wa hoja na mwenendo mzima wa Bunge na kuwahabarisha wananchi. Ninawashukuru pia madereva wetu, niwatakie wote safari njema mnaporejea majimboni kwenu.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** katikati ya mwezi huu tunatarajia kuwa na ibada za mfungo, nitumie fursa hii kuwatakia waumini wa Kiislamu maandalizi mema ya mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan na waumini wa Kikristo, maandalizi mema ya mfungo wa Kwaresma. Kwa kuwa hizo zote ni ibada muhimu kwa waumini wa madhehebu hayo ya dini, nitoe rai kwa wafanyabiashara wote kutopandisha bei za vyakula kiholela.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe rai kwa Watanzania wote kuendelea kuombea taifa letu liendelee kuwa na amani na utulivu.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo, sasa ninapenda kutoa hoja kuwa Bunge lako tukufu liahirishwe hadi **Jumanne tarehe 31 Machi, 2026** saa tatu kamili asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu hapa jijini Dodoma.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutoa hoja.